**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI MHESHIMIWA RIZIKI PEMBE JUMA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na mwisho likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liweze kuidhinisha shabaha na malengo yaliyomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukuwe nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema, uwezo na nguvu za kutekeleza yale yote tuliyojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuwezesha kukutana hapa leo tukiwa katika hali ya usalama , amani na utulivu na kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kutoa pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan na Wananchi wote wa Tanzania, kutokana na msiba mkubwa uliotokea wa kifo cha mpendwa wetu aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021. Vile vile, natoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi na Wananchi wote wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla kutokana na kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki tarehe 17 Februari, 2021. Kwa pamoja tunawaombea Mwenyezi Mungu awapumzishe Mahali pema Peponi, Amin.

4. **Mheshimiwa Spika**, baada ya salamu zangu hizo za pole, sasa napenda kutumia fursa hii adhimu kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweka historia ya kuwa Mwanamke wa kwanza kuliongoza Taifa la Tanzania na pia kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara katika wadhifa na dhamana aliyonayo kwa Taifa letu na watu wake.

   Nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Tunazidi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu awazidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yao, na daima tutapokea miongozo na maelekezo yao katika kufanikisha majukumu ya Wizara.

5. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa udhati kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa ufuatiliaji makini wa utendaji uliotukuka wa Serikali anayoiongoza. Tunampongeza na kumshukuru zaidi kwa miongozo, ushauri na nasaha anazotupatia katika kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zetu zinatoa huduma za msingi kwa Wananchi kwa ufanisi na wakati muafaka.

6. **Mheshimiwa Spika,** aidha**,** natoa shukurani kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa jitihada wanazofanya katika kumsadia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Jitihada hizo ni pamoja na ufuatiliaji wa kazi zinazotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, na Uhamasishaji wa Amani, Umoja na Mshikamano kwa Wananchi.

7. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukishukuru Chama changu, Chama Cha Mapainduzi (CCM) kwa imani kubwa iliyonionesha. Pia, nawashukuru Wanawake wote wa Mkoa wa Kaskazini

Unguja kwa imani yao kubwa kwangu kunichagua kuwa Mwakilishi na hatimae Chama kulipitisha jina langu. Nawashukuru pia viongozi wote wa CCM wa Mkoa wa Kaskazini na Jumuiya zake kwa ushirikiano wa mkubwa kwangu.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika na wasaidizi wako kwa busara na hekima unazotumia katika kuliongoza Baraza hili, namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie moyo huo. Aidha, naomba kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum kwa Ushirikiano, Ushauri, Miongozo na Maelekezo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu, nawashukuru sana.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inajumuisha Idara na Taasisi zifuatazo:-

i. Idara ya Mipango Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
iii. Afisi Kuu Pemba,
iv. Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali,
v. Mahakama ya Ardhi,
vi. Kamisheni ya Ardhi,
vii. Shirika la Nyumba Zanzibar,
viii. Wakala wa Majengo Zanzibar,
ix. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi,
x. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba,
xi. Bodi ya Kondominio,
xii. Bodi Usajili Wakandarasi,
xiii. Bodi ya Usajili Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa kazi za Kawaida na za Maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 na muelekeo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MAPATO NA MATUMIZI**

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 555.00** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato vilivyomo katika Taasisi zake, fedha hizo zinaingia katika mfuko mkuu wa Serikali . Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2021 jumla ya **TZS Milioni 535.962** zimekusanywa. Kiwango hichi ni sawa na **asilimia 96.56** ya makadirio yote. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **Kiambatisho "A".**

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara yangu ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 10.309** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara ili kufanikisha utekelezaji wa programu mbili za Wizara. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2021, Wizara yangu imepatiwa jumla ya **TZS Bilioni 4.204** ambazo ni sawa na **asilimia 40.78** na **asilimia 52.27** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9). Kati ya fedha hizo, **TZS Bilioni 1.239** kwa kazi za kawaida na **TZS Bilioni 2.964** kwa ajili ya mishahara. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **kiambatisho"B"**

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara yangu ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu mbili zifuatazo:

| | |
|---|---|
| **Programu PN0101:** | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi. |
| **Programu PN0102:** | Usimamizi wa Ardhi na Makaazi |

**PROGRAMU KUU PN0101: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI**

14. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa kazi za Wizara na inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na

Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Afisi Kuu Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 utekelezaji wa huduma za Programu hii ulikuwa kama ifuatavyo: -

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA.**

15. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 utekelezaji wa Programu hii ndogo ulilenga kutekeleza shughuli za kuratibu/ kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kuratibu uandaaji na mapitio ya Sheria za Wizara pamoja na kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta za Wizara.

16. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi wa Machi 2021 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

    i. **Uratibu na uandaaji wa mipango ya Wizara**

17. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeendelea kuratibu na kuwapeleka Maafisa Mipango 18 wa Wizara katika mafunzo ya muda mfupi (Wiki Moja) yanayohusu kuoanisha Mipango Mikuu ya Taifa, Sera za kisekta, Mpango Mkakati na Bajeti. Mafunzo hayo yaliratibiwa kutokana na kukamilika kwa kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Zanzibar ya 2020, MKUZA III na Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2015-2020. Hivyo, ilionekana umuhimu wa kuwajengea uwezo maafisa kwa ajili ya utayarishaji wa Mipango na Bajeti zinazoendana na Dira ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2020-2025 pamoja na ahadi na Hotuba za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

    Aidha, kufuatia kuanzishwa kwa Wizara mpya ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Idara imeandaa Mpango Mkakati mpya (Strategic Plan) wa miaka mitano ijayo (2021/22-2025/26) kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025, ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi wa 2020 pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar. Mpango Mkakati huo umejumuisha mapendekezo ya miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa nyumba za makaazi, nyumba za Viongozi wa SMZ na Watumishi wa Umma,

Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi kwa Miji ya Pemba (Wete, Chakechake na Mkoani) pamoja na mradi wa Utambuzi na Usajili wa Ardhi.

**ii. Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa Sera za Wizara na kuratibu mapitio ya Sheria**

18. **Mheshimiwa Spika,** katika uandaaji wa miongozo ya Kisera na Kisheria, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Taasisi zote za Wizara inaendelea na kazi ya kuzipitia Sheria zote kwa lengo la kuzifanyia marekebisho ili ziweze kuendana na hali ya sasa pamoja na kuwa na miundo na mifumo mipya ya utendaji kazi itakayoleta ufanisi zaidi wa kazi na kuondosha changamoto zinazojitokeza kwa sasa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria saba (7) za usimamizi wa Ardhi, Sheria za Usajili wa Wataalamu na Wakandarasi wa ujenzi na Sheria ya Uthamini.

Aidha, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Idara yake ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu mapitio ya Sera ya Nyumba ya 2010 na utayarishaji wa Sera ya Mipango Miji na Vijiji ambapo hatua inayoendelea ni kufanya tathmini ya hali halisi (situation analysis). Lengo ni kuhakikisha Zanzibar inakuwa na Miji ya kisasa na Makaazi bora kwa wananchi wake.

**iii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya Sekta**

19. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji (Monitoring and Evaluation) wa kazi za Wizara. Lengo la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba Mipango, Kazi na Fedha zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Miongoni mwa kazi zilizofuatiliwa ni mradi wa matengenezo ya Nyumba za Maendeleo Michenzani (Block No. 1) na matengenezo ya nyumba No. 189 – Gizenga.

Aidha, ili kuhakikisha kwamba kitengo cha ufuatiliaji kinafanya kazi kwa ufanisi zaidi, Idara imempeleka mfanyakazi wake mmoja mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Digirii ya Uzamili ya Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi (Master Degree in Project Planning,

Monitoring and Evaluation) kwa ajili ya kumuongezea utaalamu zaidi utakaoleta ufanisi wa kazi.

**iv. Kuimarisha Uhusiano baina ya Wizara za SMZ na SMT**

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza muongozo uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao umeziagiza Wizara zinazoshabihiana kimajukumu ambazo sio za Muungano, kukutana na kubadilishana uzoefu na utaalamu. Kamati ya wataalamu yenye wajumbe kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ya SMT, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi SMZ na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ya SMZ ilikutana Mjini Morogoro kwa ajili ya kuratibu Mkutano wa ngazi ya Wataalamu, Makatibu Wakuu na Waheshimiwa Mawaziri ambao ulitarajiwa kufanyika tarehe 24 - 26 Machi 2021. Hata hivyo, Mkutano huo uliakhirishwa kutokana na msiba mkubwa kutokea wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, na kwamba Mkutano huo sasa unatarajiwa kufanyika mwezi wa Juni 2021.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, jumla ya **TZS Milioni 328.670** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti. Hadi kufikia Machi 2021, fedha zilizoingizwa ni **TZS Milioni 139.880** sawa na **asilimia 42.56** na **asilimia 52.19** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

22. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inajukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara pamoja na uendelezaji wa Rasilimali Watu kwa kuandaa mipango ya kujenga uwezo wa Watumishi, kuratibu shughuli za Viongozi wa Wizara Kitaifa na Kimataifa, kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala mtambuka, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi waliopo na waliomaliza muda wao wa utumishi kwa sababu mbalimbali, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kusimamia nidhamu kwa Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake.

23. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2021, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuhakikisha ufanisi mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha ambapo Wizara imeweza kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti ya ukaguzi wa matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za Umma.

ii. Kuratibu mikutano mbali mbali ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi. Mikutano hiyo imewezesha kuleta mabadiliko, kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

iii. Kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hadi kufikia Machi 2021 Idara iliratibu mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 50 na mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 25. Kwa ufafanuzi zaidi angalia **kiambatisho "C1 na C2 ".**

iv. Katika kutekeleza Mpango wa Rasilimali Watu, Idara iliratibu uajiri wa wafanyakazi 37 kwa ajili ya kujaza nafasi zilizokuwa wazi na nafasi mpya pamoja na uajiri wa wataalamu. Aidha, Idara iliwapatia mafunzo ya awali ya kuingia kazini (induction course) wafanyakazi hao ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa uweledi na ufanisi kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi Serikalini.

v. Kufanya malipo ya huduma za uendeshaji wa Afisi yakiwemo malipo ya maji, umeme, ununuzi wa samani, kompyuta tatu (3) na vifaa vya kuandikia (stationaries) pamoja na ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri vya Wizara ambapo jumla ya Gari nne (4) zimekatiwa bima, Gari tano (5) na Vespa mbili (2 )kufanyiwa matengenezo madogo madogo.

vi. Kulipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo kuwapatia posho za likizo wafanyakazi ishirini (20), malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi ishirini na sita (26), kutoa ubani wa kufiwa kwa wafanyakazi watano (5).

vii. Kuratibu na kutoa misaada kwa wafanyakazi wenye mahitaji maalumu na kusaidia utoaji wa elimu katika masuala mtambuka ikiwemo UKIMWI, Rushwa na Maradhi ya kuambukiza kama vile ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya Korona (**Covid19).**

**24.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS Bilioni 2.155** kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Uendeshaji na Utumishi. Hadi kufikia Machi 2021, fedha zilizoingizwa ni **TZS Bilioni 1.171** ambazo ni sawa na **asilimia 54** na **asilimia 65.30** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

25. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba na inajukumu la kuratibu na kusimamia utawala na mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufika Machi, 2021 programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kusimamia na kuratibu shughuli za uendeshaji na utawala za kila siku kwa kulipia gharama za ununuzi wa vifaa vya kuandikia, malipo ya huduma za umeme, maji, mtandao, simu, gharama za posta na matengenezo ya vyombo vya usafiri.
ii. Kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia stahiki zao ikiwemo malipo baada ya saa za kazi (over time) kwa wafanyakazi kumi na saba (17) na stahiki za likizo kwa wafanyakazi wanne (4). Aidha kuwajengea uwezo na mazingira mazuri wafanyakazi wa Afisi Kuu Pemba.
iii. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida zinazotekelezwa na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba kama vile upangaji wa Miji, Upimaji wa Viwanja vinavyotokana na maombi ya wananchi kwa maeneo yao binafsi, Upimaji wa mashamba ya Eka Tatu, utayarishaji wa ramani za maeneo ya viwanja na mashamba yaliyopimwa, utayarishaji na utoaji wa hati za matumizi ya Ardhi, kazi za Uthamini, Utambuzi na Usajili wa Ardhi kwa maeneo mbali mbali katika Wilaya ya Wete na Wilaya ya Chakechake, usimamizi wa matengenezo ya nyumba (Block) namba 4 Madungu, nyumba za Kipangani na nyumba za *Police line* Wete.

26. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS Milioni 612.302** kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wake. Hadi kufikia Machi 2021, fedha zilizoingizwa ni **TZS Milioni 487.285** ambazo sawa na **asilimia 79.582** na **asilimia 98.75** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU KUU PN0102: USIMAMIZI WA ARDHI NA MAKAAZI**

27. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na huduma za makaazi bora kwa Wananchi na inajumuisha Programu ndogo mbili kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI**

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mahakama ya Ardhi ambapo Mahakama ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 1994. Shughuli za msingi za Mahakama hii ni kupokea, kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokona na migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali.

29. **Mheshimiwa Spika,** tangu Mahakama hii kuanza kazi mwaka 2006 hadi Machi 2021, jumla ya migogoro 3,603 imepokelewa ambapo kwa Unguja ni migogoro 2,125 na Pemba ni migogoro 1,485. Kwa upande wa usuluhishi, jumla ya migogoro 3384 imepatiwa ufumbuzi sawa na asilimia 94 ya migogoro yote ya ardhi iliyopokelewa na Mahakama ya Ardhi.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Mahakama ya Ardhi kupitia Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. **Utatuzi wa migogoro ya ardhi**

31. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Mahakama ya Ardhi imepokea kesi mpya 139 ambazo zilifunguliwa Unguja na Pemba. Mahakama imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi 132 zilitolewa uamuzi na jumla ya kesi 218 zinaendelea katika Mahakama ya Ardhi Unguja na Pemba kama inavyoonekana katika Jaduweli nambari 1:

***Jaduweli Nambari 1: kesi zilizopokelewa na kutolewa Maamuzi Januari – Machi 2021***

| Sn | MKOA | KESI MPYA ZILIZOPOKELEWA | KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|---|
| | Mjini Magharibi | 28 | 21 | 51 |
| | Kaskazini Unguja | 55 | 53 | 88 |
| | Kusini Unguja | 15 | 08 | 30 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini Pemba | 18 | 21 | 29 |
| | Kusini Pemba | 23 | 29 | 20 |
| | **JUMLA** | **139** | **132** | **218** |

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha utoaji wa huduma nzuri kwa Wananchi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, Mahakama ya Ardhi imehama katika jengo liliopo Majestick ambalo lilikua katika hali mbaya inayohatarisha usalama wa wafanyakazi na wananchi waliokua wanakwenda kusilikiza malalamiko yao. Mahakama ya Ardhi kwa sasa imehamia Mwanakwerekwe katika jengo ambalo lilikua linatumiwa na Idara ya Nishati na Madini, Jengo ambalo Wizara tayari imelifanyia ukarabati na kuwezesha mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi na wananchi wanaofika kupata huduma zinazotolewa na Mahakama hiyo.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua mbalimbali za kutafuta ufumbuzi kwa baadhi ya migogoro mikubwa ya ardhi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imekua karibu sana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri na miongozo ya kisheria. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano anaotupatia.

34. **Mheshimiwa Spika,** mbali na kesi zinazowasilishwa Mahakama ya Ardhi, Wizara kupitia utaratibu wake wa kukutana na Wananchi katika siku za Jumanne na Alhamis kila Wiki na ziara mbalimbali zinazofanywa na Viongozi katika maeneo ya migogoro hasa ya muda mrefu, hadi kufikia Machi 2021 imepokea migogoro ya ardhi 237 kwa Unguja na Pemba, ambapo migogoro 74 imetatuliwa na migogoro 163 imetolewa maelekezo ya awali na inaendelea kwa uchunguzi wa kina. Aidha, kwa kuongeza ufanisi na ufumbuzi wa haraka wa migogoro ya ardhi inayowasilishwa Wizarani, Wizara imeunda Kamati Maalumu ambayo inajumuisha Wanasheria na Wapimaji Ardhi. Kamati hiyo hufanya ziara za kukutana na walalamikaji na wanaolalamikiwa pamoja na wananchi wa eneo husika kwa lengo la kupata taarifa za kina na zinazojitosheleza na kuishauri Wizara hatua stahiki za kuchukuliwa katika utatuzi wa migogoro hiyo. Hatua hii imesaidia sana kuweza kupata ufumbuzi wa haraka hasa migogoro ya ardhi ya muda mrefu.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 jumla ya **TZS Milioni 668.874** zilipangwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu hii. Hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 241.157** sawa na **asilimia 36.05** na **asilimia 42.11** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI NYUMBA NA MAKAAZI**

36. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 utekelezaji wa Programu hii ndogo ulilenga katika kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi na uimarishaji wa huduma za makaazi kupitia upimaji wa ardhi, utambuzi na usajili wa ardhi, mipango miji na matumizi ya ardhi, ukarabati wa nyumba za maendeleo na majengo ya Serikali. Programu hii ndogo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo:-

**KAMISHENI YA ARDHI**

37. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia Sheria za Sekta ya Ardhi pamoja na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi.

**MAPATO NA MATUMIZI**

38. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kamisheni ya Ardhi (COLA) ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Milioni 535.00** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia Machi 2021, Kamisheni imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 521.820** ambazo ni sawa na **asilimia 97.536** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, jumla ya **TZS Bilioni 2.776** ziliidhinishwa kutumika ambapo **TZS Bilion 1.120** ni ruzuku ya kazi za kawaida na **TZS Bilioni 1.656** rukuzu ya mishahara. Hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **TZS Milion 188** kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 16.8** na **TZS Bilioni 1.205** ruzuku ya mishahara sawa na **asilimia 72.8.** Hivyo kufanya jumla ya fedha zote zilizoingizwa kwa Kamisheni ya Ardhi kuwa ni **TZS Billion 1.392** sawa na **asilimia 50.18** na **asilimia 66.88** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**39. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Kamisheni ya Ardhi ilitekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

**i. Utawala na uendeshaji**

a) Kuwajengea uwezo wafanyakazi ambapo jumla ya wafanyakazi 22 wamepatiwa mafunzo ya ndani yanayohusu utayarishaji wa Hati za Ardhi na wafanyakazi 26 wamepatiwa mafunzo tofauti ya utendaji wa majukumu yao.

b) Kusimamia maslahi ya Wafanyakazi ambapo stahiki zimetolewa kwa wafanyakazi 45 ikiwemo likizo na malipo baada ya saa za kazi.

**ii. Ugawaji na usimamizi wa ardhi**

a) Kutayarisha Hati 574 ambapo Hati 429 kwa Unguja na Hati 145 kwa Pemba.
b) Kutayarisha Mikataba 191 ya Ukodishaji Ardhi ambapo Mikataba 177 kwa Unguja na Mikataba 14 kwa Pemba.
c) Kufanya ukaguzi wa maeneo 81 ya Ardhi za Eka Tatu na maeneo 180 ya Ardhi za Ukodishwaji.
d) Kutayarisha vitambulisho 106 vya Matumizi ya Ardhi ya Eka Tatu.
e) Jumla ya kazi za uthamini 309 zilifanywa ambapo 236 kwa Unguja na 73 kwa Pemba. Kazi hii hutegemea idadi ya maombi yaliyowasilishwa ya kutaka kufanyiwa kazi kwa madhumuni mbalimbali yakiwemo ya mirathi, kujua thamani ya mali na ulipaji fidia.
f) Kufanya utambuzi wa maeneo 633 ambapo maeneo 517 kwa Unguja na 116 kwa upande wa Pemba

**iii. Kuratibu na kusimamia usajili wa ardhi**

a) Kuhakiki maeneo 611 ambapo kwa Unguja ni maeneo 511 na kwa Pemba maeneo 100. Maeneo hayo ni kwa Wilaya za Mjini, Magharibi A na B, Chake Chake, Wete na Mkoani.
b) Kusajili maeneo (parcels) 419 ambapo maeneo 399 kwa Unguja na 20 kwa Pemba Maeneo hayo yaliyosajiliwa ni kwa Wilaya za Mjini, Magharibi A na B, Chake Chake, Wete, Mkoani na Micheweni.

c) Jumla ya hati za ardhi 783 zimelipiwa ada ya usajili wa ardhi ambapo kwa Unguja ni 684 na Pemba ni 99.

d) Kuweka taarifa za mabadiliko ya umiliki wa matumizi ya ardhi kwa ardhi zilizosajiliwa. Afisi ya Mrajis wa Ardhi imeweza kusajili maeneo 31 ambapo kwa Unguja ni maeneo 29 na kwa Pemba ni maeneo 2.

e) Jumla ya kadi za usajili wa ardhi 290 zimetengenezwa ambapo kwa Unguja ni kadi 155 na Pemba ni kadi 135

f) Kutayarisha Rejista 1 kwa Shehia ya Jang'ombe Urusi.

g) Kutoa elimu ya uhamasishaji wa Usajili wa Ardhi. Jumla ya mikutano 8 imefanyika ambapo 3 ni kwa Unguja na 5 ni Pemba.

h) Semina 16 za mafunzo kwa wafanyakazi zimeendeshwa ambapo 13 ni Unguja na 3 Pemba. Mafunzo hayo yalilenga katika kuwajengea uwezo ili kuwa weledi katika utendaji wa kazi.

i) Makala 8 zimetayarishwa kwa ajili ya kuchapishwa katika Jarida la ARDHI toleo la tano.

**iv. Upimaji na utoaji wa ramani za ardhi**

a) Jumla ya viwanja 839 vimepimwa ambapo 610 kwa upande wa Unguja na 229 kwa upande wa Pemba kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

b) Jumla ya maeneo 144 yalipimwa kutokana na maagizo ya Serikali. Kati ya hayo, maeneo 10 ni kwa Unguja na 134 kwa Pemba.

c) Kuweka alama za Upimaji (control points) 30 katika mfumo wa komputa.

d) Jumla ya ramani za ardhi 1,934 zimetayarishwa ambapo 1,706 kwa Unguja na 228 kwa Pemba.

**v. Upangaji wa miji na matumizi ya ardhi**

a) Kutoa miongozo ya ujenzi (Planning Policy Guidelines - PPG) 555 ambapo Unguja ni 453 na Pemba 102 sambamba na kutoa vibali vya ujenzi 547 (Unguja 446 na Pemba 101).

b) Kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa kitovu cha Mji wa Zanzibar (Zanzibar City Centre-Local Area Plan) kwa kusimamia mradi wa "Green-Corridor".

c) Kupanga maeneo matatu (3) ya wazi (Open spaces) sambamba na kupanga miji midogo miwili (2) kwa Unguja na mmoja (1) kwa Pemba. Miji hiyo ni Fumba na Dunga kwa upande wa Unguja, na Finya kwa upande wa Pemba.

d) Mikutano mitatu (3) iliyowashirikisha washirika wa mipango miji ilifanyika kwa ajili ya kujadiliana Mpango wa Mji wa Micheweni.

e) Kuendelea na hatua za utayarishaji wa Sera, Sheria na Kanuni mpya za Mipango Miji na Maendeleo ya Ardhi.

**BODI YA UHAULISHAJI ARDHI**

**40.** **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi (Land Transfer Board) imeanzishwa kwa Sheria Namba 8 ya Mwaka 1994. Lengo la kuanzishwa Bodi hii ni kupokea na kusikiliza maombi ya Uhaulishaji wa ardhi na kusajili ardhi hiyo baada ya kuhaulishwa.

**MAPATO NA MATUMIZI**

**41.** **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Bilion**i **2.8** ambapo hadi kufikia Machi, 2021 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.7** sawa na **asilimia 60.714** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ilikadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1.717** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS Mil 211** sawa na asilimia **12.29 na asilimia 16.38** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**42.** **Mheshimiwa spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Bodi ya Uhaulishaji Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Jumla ya fomu 2,426 za Uhaulishaji wa Ardhi zilitolewa kwa Wananchi waliohitaji kufanya uhaulishaji wa ardhi (land transfer).

ii. Jumla ya maombi 1,987 ya Uhaulishaji wa Ardhi yamepokelewa ambapo maombi yaliyokubaliwa ni 1,023, maombi yaliyorejeshwa na kutolewa maelekezo ya hatua za kuchukua ni 840 na maombi yalioyokataliwa ni 124.
iii. Jumla ya ziara 22 za ukaguzi wa maeneo yaliyoombewa kufanyiwa uhaulishaji zimefanyika.
iv. Kutoa elimu inayohusiana na Uhaulishaji wa Ardhi kwa Wilaya 4 za Pemba. Elimu hiyo imetolewa kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Masheha.
v. Watendaji watatu (3) na wajumbe watano (5) wa Bodi wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Saalam katika fani ya Urasimishaji wa Miji isiyo rasmi na fani ya Utawala na Usimamizi wa Ardhi.

**OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

**43. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya mwaka 2015 kwa dhumuni la kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na wathamini wa Taasisi za Serikali na Kampuni binafsi. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:-

**i. Kupitisha na kuthibitisha ripoti za uthamini wa rasilimali kwa madhumuni mbalimbali.**

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 jumla ya ripoti 221 zimethibitishwa ambapo 88 ni ripoti za uthamini kwa ajili ya mikopo (Morgage purpose), 35 ni ripoti za uthamini kwa ajili ya thamani (Market Value Determination), 52 ni ripoti za uthamini kwa ajili ya mirathi (Inheritance purpose) na 46 ni ripoti za uthamini kwa ajili ya fidia (Compensation purpose). Utekelezaji wa Shughuli hii hutegemea maombi yanayowasilishwa.

**ii. Kutayarisha ripoti ya shughuli za uthamini kwa kila robo Mwaka.**

45. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetoa Ripoti ya Shughuli zote za uthamini kwa kila robo Mwaka. Ripoti hiyo inaonesha kazi ambazo Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imezifanya kwa kipindi cha robo husika pamoja na changamoto zake.

**iii. Kutayarisha na kuingiza taarifa za mali zilizofanyiwa Uthamini katika mfumo wa Kieletroniki.**

46. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imekamilisha utayarishaji wa mfumo wa kieletroniki (data base) unaotumika kuweka taarifa za mali zinazofanyiwa uthamini. Mfumo huo unasaidia kutunza taarifa muhimu za kazi za uthamini zinazoletwa kwa ajili ya kuhakikiwa na kuidhinishwa.

**iv. Kufanya uhamasishaji kwenye Skuli za Sekondari kusoma fani za Ardhi.**

47. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa na wataalamu wa kutosha katika fani za Usimamizi wa Ardhi na Uthamini kwa siku za baadae, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imefanya zoezi la kuhamasisha wanafunzi kusoma fani hizo wanapojiunga na vyuo vikuu na vyuo vya kati. Uhamasishaji huo hufanyika kwa wanafunzi wa kidato cha nne hadi cha sita. Zoezi hili limefanyika kwa skuli za Serikali na binafsi ambapo kwa Unguja ni Skuli 16 na Pemba ni Skuli 6.

**v. Kufanya mapitio ya Sheria ya Usajili wa Wathamini**

48. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya mapitio (review) ya Sheria ya Usajili wa Wathamini Namba 5 ya mwaka 2015 ili iweze kukidhi matakwa ya sasa. Mapitio hayo yanalenga kuanzisha mfumo mpya wa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na kuimarisha Bodi ya Usajili wa Uthamini ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na Wananchi kwa ujumla.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 jumla ya **TZS Milioni 132.00** ziliidhinishwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Mthamini Mkuu wa

Serikali. Hadi kufikia Machi 2021, fedha zilizoingizwa ni **TZS Milioni 40.882** sawa na **asilimia 30.97** na **asilimia 41.29** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

**50. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa Tangazo la Kisheria (Legal Notice) namba 50 ya mwaka 2017. Lengo la kuanzishwa Wakala wa Majengo ni kutoa huduma ya Makaazi kwa Viongozi Wakuu, Maafisa Wakuu Waandamizi wa Serikali na Watumishi wa Umma. Aidha, Wakala wa Majengo ina wajibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo.

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Taasisi yake ya Wakala wa Majengo imetayarisha Mpango Mkakati wa Miaka Mitano pamoja na Muundo wa Taasisi kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha Wakala wa Majengo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 iliendelea na kazi za usimamizi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Taasisi za Serikali kama ifuatavyo:-

i. Kutayarisha ramani, BOQ na nyaraka za zabuni (Pre-Contract)
ii. Kusimamia kazi za ujenzi (Post-Contract)
iii. Kutayarisha ramani, BOQ, nyaraka za zabuni pamoja na kusimamia ujenzi (Pre-Contract and Post-Contract)
iv. Miradi ya ukarani (Clerk of Work)

**52. Mheshimiwa Spika,** jumla ya miradi 49 imefanyiwa kazi na ipo katika hatua tofauti kama inavyoonekana katika **Kiambatisho "D".**

**53. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wakala wa Majengo ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 380.01** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2021 jumla ya **TZS Milioni 93.956** zimetumika ambazo ni sawa na **asilimia 24.72** na **asilimia 32.51** ya ulinganisho wa Fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

**54.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) limeanzishwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2014. Lengo la kuanzishwa Taasisi hii ni kuwawezesha Wananchi kupata makaazi bora na salama pamoja na kuziimarisha nyumba za Shirika zilizopo na kujenga nyumba mpya.

**MAPATO NA MATUMIZI**

**55.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Shirika lilikadiria kukusanya Jumla ya **TZS Bilioni 3.035.** Hadi kufika Machi 2021, jumla ya **TZS Bilioni 2.059** zimekusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 67.84** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilikadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 2.855** ambapo hadi kufikia Machi 2021 jumla ya **Bilioni 1.652** zimetumika ambazo ni sawa na **asilimia 57.868** ya makadirio.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Shirika la Nyumba limetekeleza kazi zifuatazo:

**i. Matengenezo ya nyumba za Shirika**

a) Matengenezo ya awamu ya kwanza (Phase I) ya nyumba za maendeleo 36 za Bloki No. 1 Michenzani yamekamilika.
b) Matengenezo ya awamu ya pili (Phase II) ya nyumba za maendeleo 24 za Bloki No. 1 Michenzani yataanza mara tu baada ya kutiliana Mkataba na Mkandarasi ambaye ni Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).
c) Zabuni ya matengenezo ya nyumba namba 1699/1705 Mnadani imetangazwa na matengenezo hayo yataanza baada ya taratibu za kumpata Mkandarasi kukamilika.
d) Matengenezo ya nyumba namba 189-Gizenga yanaendelea na yamefikia 75% ya kukamilika kwake.
e) Matengenezo ya nyumba za Kikwajuni yamefanyika kwa kuezeka Blocki I na Block K na matengenezo ya nyumba nambari 293 iliyopo Kiponda (Phase I) yamekamilika.

f) Matengenezo ya kipaa cha ngazi ya bloki No.1 Kilimani yanaendelea.

g) Michoro ya ujenzi wa jengo la makaazi na biashara Kiembe Samaki imeanza kuchorwa.

h) Matengenezo ya nyumba 10 (block number 3) za Maendeleo Madungu yamekamilika.

i) Matengenezo ya nyumba 8 (Block no. 2 na block no.5) za Maendeleo Madungu yanaendelea.

j) Matengenezo ya nyumba T 15-Kilimatinde, no. 18/A, 1/35, T10/D za Wete na no. S.M.Z. 14A, SMZ, 19 na SMZ 27 za Police Line Wete yamekamilika.

**ii. Kuzitambua, kuzithamini na kuziorodhesha milki za Shirika**

a) Shirika linaendelea na Uthamini wa nyumba zake zilizopo Mji Mkongwe.

b) Kubandika vibati vya nambari kwenye nyumba za Shirika katika maeneo ya Vuga, Kajificheni, SokoMuhogo, Malindi na Kokoni imekamilika.

**iii. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi**

a) Wafanyakazi kumi na tano (15) wa fani tofauti wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

b) Shirika limenunua piki piki mbili (2) kwa ajili ya kurahisisha utendaji na ufuatiliaji wa kazi za Shirika kwa upande wa Pemba.

**iv. Kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato ya Shirika**

a) Kufanya ukaguzi wa kawaida wa mara kwa mara wa nyumba za Shirika ili kuwatambua wapangaji halisi, kufuatilia madeni, mikataba ya upangishwaji na kujua changamoto zilizopo.

b) Wizara kupitia Shirika la Nyumba imekuwa ikihamasisha wapangaji wake kupitia mikutano na wapangaji, matangazo katika vyombo vya habari na kutoa barua za ukumbusho wa kulipa kodi za nyumba ili kuongeza makusanyo na kuliwezesha Shirika kujiendesha.

c) Kutoa mikataba 340 ya ukodishaji kwa wapangaji wa nyumba za Shirika.

d) Kuratibu mikutano ya wapangaji wa nyumba za Shirika kwa maeneo ya Mombasa, Saateni, Mji Mkongwe na Gamba.

**BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA**

57. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya kudhibiti Kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Sura ya 98 ya mwaka 1953 (CAP 98 of 1953). Lengo la kuanzishwa kwa Bodi hii ni kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokana na migogoro ya upangishaji wa nyumba za Serikali na nyumba binafsi.

58. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza yafuatayo:-

    i. Imepokea mashauri 18, kati ya hayo Unguja 15 na Pemba 3.
    ii. Imeweza kusikiliza mashauri 33 kwa Unguja na Pemba.
    iii. Imeweza kuyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya kodi za nyumba kwa Zanzibar yapatayo 11 ambayo kwa Unguja ni 9 na Pemba 2.

59. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 186** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 42.035** ambazo ni sawa na **asilimia 22.60** na **asilimia 29.51** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**BODI YA KONDOMINIO**

60. **Mheshimiwa Spika,** Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Kondominio namba 10 ya mwaka 2010. Lengo la kuanzishwa Bodi ya Kondominio ni kusajili, kuratibu na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na watu tofauti.

61. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Bodi ya Kondominio ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 200.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Hadi kufikia mwezi Machi 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 51.30** ambazo ni sawa na **asilimia 25.65** na **asilimia 34.20** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

62. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi machi 2021 Bodi ya Kondominio imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuwajengea uwezo wajumbe wa Bodi kupitia Kongamano la Jumuiya ya Wataalamu wa Milki za Nyumba Tanzania "Association of Real Estate Professionals of Tanzania (AREPTA)'' ambalo lilitoa elimu na kujadili masuala mbali mbali ya Sekta ya milki za Nyumba.

ii. Kufanya vikao vya uelimishaji kwa Masheha wa Wilaya ya Magharibi B na kwa Wakaazi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani (Bloki Nam. 1) kuhusu dhana ya Kondominio pamoja na utaratibu wa usajili na usimamizi wa Majengo ya Kondominio.

iii. Kutayarisha na kutumia mfumo maalumu wa kuhifadhi kumbukumbu za usajili (Registration data base). Kwa sasa Ofisi imetengeneza mfumo wa uhifadhi kumbukumbu wa kawaida hadi mfumo maalumu utakapokamilika

iv. Kufanya ziara ya kikazi na kukutana na Mkuu wa Wilaya ya Mjini kujadiliana masuala ya Kondominio pamoja na kuandaa utaratibu wa kuanza kazi za usajili wa Kondominio kwa Wilaya Mjini.

v. Kufanya ukaguzi katika maeneo ya miradi iliyowasilisha maombi ya usajili wa Kondominio. Miradi hiyo ni pamoja na Zanzibar Villa Ltd uliopo Paje, Zanzibar Social Security Estate uliopo Mbweni, Balladin Ltd uliopo Uroa na Nyumba za Maendeleo Michenzani.

vi. Kufanya usajili wa ramani ya mradi wa Zanzibar Villa Ltd uliopo Paje na mradi wa Balladin Ltd – Uroa.

vii. Bodi inaendelea kufanya uchambuzi na uhakiki wa maombi mbalimbali ya usajili kupitia Kamati Maalumu.

viii. Kutayarisha na kuanza kutumia Daftari la Usajili wa Kondominio (Condominium Register).

ix. Kuendelea na hatua za usajili wa Majengo ya Kondominio kwa Nyumba 132 za Block Nambari 1 Michenzani

x. Kutayarisha na kusanifu vipeperushi, “rollup”, “flier”, “banner” ambavyo vitatumika katika kutangaza Bodi na kutoa elimu kuhusu dhana ya Kondominio na umuhimu wa usajili na matunzo ya majengo ya Kondominio.

xi. Kufanya vikao viwili vya kawaida ambavyo vilijadili utekelezaji wa kazi na kupitisha maazimio mbalimbali ya kufanikisha majukumu ya Bodi.

xii. Kutoa huduma za uendeshaji wa Afisi ambapo Bodi imefanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi kama vile kuzibua makaro na kutengeneza mifuniko ya makaro pamoja na kutia “Aircondition” katika Ofisi ya Mrajis, Kulipa nusu ya gharama ya ununuzi wa chombo cha usafiri cha aina ya Click, kununua Vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

**BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO**

63. **Mheshimiwa Spika,** Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo namba 5 ya Mwaka 2008. Lengo la kuanzishwa kwa Bodi hii ni kusimamia, kudhibiti na kuwaendeleza wataalamu wa ujenzi ili wafanye kazi zao kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa.

**MAPATO NA MATUMIZI**

64. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Bodi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Milioni 330.585** ambapo hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizokusanywa ni **TZS 248.178** sawa na **asilimia 75.07** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi Bodi ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 793.280** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021 Bodi imepatiwa jumla ya **TZS Milioni 128.730** sawa na **asilimia 16.23 na asilimia 21.64** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

65. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kusajili wataalamu bingwa wazalendo 8, Wataalamu wa kigeni 3, Mtaalamu Ushauri 1, Wahitimu 33 na Mafundi 4.
ii. Kusajili kampuni za saba (7) za Ushauri za ndani ya nchi (Kizalendo) na Kampuni moja (1) ya kigeni.
iii. Kusajili miradi 154 ya ujenzi kwa Unguja na Pemba. Miradi hiyo inajumuisha Majengo ya biashara, Nyumba za makaazi, Hoteli, Skuli, Nyumba za Ibada na mengineyo.
iv. Kufanya ukaguzi katika maeneo 64 ya Ujenzi kwa Unguja na Pemba.
v. Kufanya warsha iliyojadili kuwaendeleza wahitimu na uanzishwaji wa utoaji wa leseni za kufanyia kazi kwa wataalamu waliosajiliwa na Bodi. Mkutano huo uliwahusisha wahitimu na wataalamu wa ujenzi kutoka Sekta binafsi na Serikali kwa lengo la kutoa elimu juu ya umuhimu wa kusajili Wataalamu wake pamoja na kuwapa dhamana za kusimamia majengo kwa mujibu wa Sheria.

Vilevile Bodi imetekeleza takwa la kisheria la kuanzishwa kwa utoaji wa leseni za kazi (Practise Licence) kwa Wataalamu waliosajiliwa na Bodi sambamba na kuzindua Mpango wa kuwaendeleza Wataalamu kwa kufikia alama maalum (Point Development Units) na Mpango wa miaka mitatu wa Kuwaendeleza Wahitimu (Structure Apprentiship Programme) ikiwemo kuwapatia maeneo ya kuweza kufanya mafunzo ya vitendo kwa kuwapangia kwenye kampuni za ujenzi na hatimae tuweze kupata Watalamu bora mara baada ya kumaliza mpango huo.

**BODI YA USAJILI WAKANDARASI**

66. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili Wakandarasi imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wakandarasi namba 6 ya mwaka 2008. Lengo la kuanzishwa Bodi hii ni kusimamia kampuni za ujenzi (Wakandarasi) na miradi ya ujenzi inayotekelezwa nchini ili kuzingatia viwango na usalama.

**MAPATO NA MATUMIZI**

**67. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bodi hii ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Milioni 519.183** ambapo hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 305.562** ambazo ni sawa na **asilimia 58.85**4 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bodi hii ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 359.601** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 203.655** sawa na **aslimia 56.63** na **asilimia 75.51** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Bodi ya Usajili Wakandarasi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kusajili Wakandarasi wapya 38 ambapo kati ya hao Wakandarasi 14 ni Wageni, 16 kutoka Tanzania Bara na 8 kutoka Zanzibar,
ii. Kufanya ukaguzi kwa Wakandarasi wapya kumi na nane (18) ambao waliwasilisha maombi ya kusajiliwa. Maombi hayo yalihusisha Wakandarasi kumi na sita (16) kutoka Unguja na wawili (2) kutoka Pemba.
iii. Kufanya ziara za ukaguzi kwa maeneo 86 ya miradi ya ujenzi ambapo maeneo 72 kwa Unguja na 14 kwa Pemba. Aidha, Bodi iliendesha vikao 39 kwa Unguja na 14 kwa Pemba vinavyohusiana na kesi kwa wanaokwenda kinyume na Sheria na Kanuni za Bodi.
iv. Kuwatunuku zawadi vijana waliomaliza kidato cha sita na kufaulu vizuri kwa alama ya "**A**" kwenye masomo ya hesabati na fizikia.
v. Kushiriki katika Kongamano la Jumuiya ya Wataalamu wa Milki za Nyumba Tanzania "Association of Real Estate Professionals of Tanzania (AREPTA)" kwa lengo la kuwajengea uwezo wajumbe wa bodi kuhusiana na masuala ya "Real Estate".

**MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**69. Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, sasa naomba kuwasilisha muelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia Programu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**70. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 19.117** ambapo **TZS Bilioni 8.807** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida, na **TZS Billioni 10.310** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida jumla ya **TZS Bilioni 2.396** ni kwa ajili ya mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1.167** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 5.243** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara. Aidha, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS Bilioni 1.294** zinazoingia katika mfuko Mkuu wa Serikali.

**71. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepanga kutekeleza majukumu yake ya msingi kupitia Programu Kuu tatu zifuatazo:-

a. **Programu PN0201:** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.
b. **Programu PN0202:** Usimamizi wa Ardhi
c. **Programu PN0203:** Maendeleo ya Makaazi

**72. Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kuhusu Programu Kuu na Programu ndogo zinazohusiana na Wizara yangu kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

73. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kusimamia na kuratibu Mipango Mikuu ya Wizara, Sera na Tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji wa rasilimali katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa katika programu hii ni kukuza ufanisi katika usimamizi wa mipango na utawala wa rasilimali pamoja na utoaji wa huduma za kijamii. Programu hii itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla ya **TZS Bilioni 2.980** zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wake. Programu hii imegawanyika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

74. **Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu ndogo hii ni uratibu na usimamizi wa Mipango Mikuu ya Wizara kwa ufanisi ambayo itasimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Programu hii imepanga kuandaa Mipango ya muda mfupi na mrefu ya Wizara, kuratibu mapitio na kuandaa Sera ya Nyumba na Sera ya Mipango Miji, kuratibu mapitio ya Sheria zote zilizo chini ya Taasisi za Wizara, Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Wizara na kufanya tafiti kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma bora katika sekta za Wizara.

75. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 305.400** kwa kazi za kawaida na mishahara.

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

76. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kusimamia Uendeshaji na Utawala katika Sekta za Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo inajukumu la kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi na Maendeleo ya Wafanyakazi, Wajibu na maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Programu hii imepanga kuendeleza utoaji wa huduma za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa, kujenga uwezo wa wafanyakazi na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za utumishi, kufanya mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya

Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa.

**77. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii ndogo kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. Bilioni 1.928** kwa kazi za kawaida na mishahara.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

**78. Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu hii ni Uratibu, Usimamiaji na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba. Programu ndogo hii inajukumu la kuhakikisha malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi zaidi. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 huduma zinazotarajiwa kutolewa ni pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa Pemba, uratibu wa utekelezaji wa Mipango, Sera, Tafiti pamoja na kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wote katika Afisi kuu Pemba.

**79. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii ndogo kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naliomba Baraza lakoTukufu kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 746.60** kwa kazi za kawaida na mishahara.

**PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI**

**80. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi (Security of Land Tenure). Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora na fanisi. Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Ardhi, ambapo jumla ya **TZS Bilioni 4.218** zinatarajiwa kutumika.

**81. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imegawanyika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI**

**82. Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu ndogo hii ni kuhakikisha usalama wa umiliki wa Ardhi na mipango bora ya usimamizi wa matumizi ya ardhi nchini. Matokeo ya muda mfupi (output) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kutatua na

kupungua kwa migogoro ya ardhi, ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa matumizi mbali mbali, uthamini wa ardhi, usajili wa ardhi, usimamiaji wa shughuli za upimaji na ramani, upangaji wa miji na matumizi ya ardhi.

**MAHAKAMA YA ARDHI**

**83. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Mahakama ya Ardhi kupitia programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuongeza ufanisi na kasi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi kwa lengo la kuzitolea maamuzi kesi 260 kwa mwaka kwa Unguja na Pemba.
ii. Kuendelea na matengenezo ya jengo la Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Mjini Magharibi (Mwanakwerekwe) ili liendane na shughuli za Mahakama.
iii. Kufanya matengenezo ya paa la jengo la Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Kusini Unguja (Koani).
iv. Kujenga uzio (fence), mnara wa tangi la maji pamoja na choo cha nje katika jengo la Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Kaskazini Unguja (Gamba).
v. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na kazi za Mahakama ya Ardhi juu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na kutoa elimu kwa jamii ili kuepuka kujiingiza kwenye migogoro ya ardhi kwa kufuata Sheria za Ardhi na Mazingira kabla ya utumiaji Ardhi.

**KAMISHENI YA ARDHI**

**84. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamisheni ya Ardhi katika Programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi watano (5) na muda mrefu wafanyakazi watano (5).
ii. Kulipa stahiki kwa wafanyakazi 70 ikiwemo likizo na malipo baada ya saa za kazi.
iii. Matengenezo ya jengo la Kamisheni na Kuendelea kusimamia shughuli za uendeshaji.

iv. Kutayarisha hati za Haki ya Matumizi ya Ardhi 1,900, Mikataba 140 ya Ukodishaji Ardhi, na Vitambulisho 100 vya matumizi ya Ardhi za Eka Tatu pamoja na kuingiza taarifa zake katika Mfumo wa kompyuta.

v. Kuendeleza ukaguzi wa maeneo 150 ya uwekezaji na maeneo 150 ya Eka Tatu za Ardhi za Kilimo Unguja na Pemba .

vi. Kufanya kazi za Uthamini wa Ardhi kwa maeneo 350 kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

vii. Kuendelea na zoezi la kuwatambua wenye Haki ya Matumizi ya Ardhi kwa viwanja 2,000.

viii. Usimamiaji wa shughuli za upimaji wa viwanja 1,625 nchini.

ix. Utayarishaji wa Ramani 1,000 za Ardhi pamoja na utoaji wa taarifa 12 za kupwa na kujaa kwa maji ya bahari.

x. Kufanya uhakiki wa maeneo ya ardhi 1,500 (Unguja maeneo 1,000 na kwa Pemba maeneo 500).

xi. Kusajili maeneo ya ardhi 1,500 (Unguja ni maeneo 1,000 na Pemba ni maeneno 500).

xii. Idadi ya hati zitakazolipiwa na wananchi ni 1000 ambapo kwa Unguja ni hati 800 na kwa upande wa Pemba ni hati 200.

xiii. Idadi ya maeneo yatakayoendelezwa kiusajili ni 80 ambapo kwa Unguja ni 60 na kwa upande wa Pemba ni 20.

xiv. Idadi ya mikutano ya uhamasishaji wa usajili wa ardhi itakayofanyika ni 20 ambapo 12 ni kwa upande wa Unguja na Pemba ni 8.

xv. Kutayarisha Marejista ya Shehia 8 (Unguja ni 4 na Pemba ni 4).

xvi. Kutayarisha kadi za usajili 1,300 (Unguja 1,000 na Pemba ni 300).

xvii. Kufanya semina na mafunzo kwa wafanyakazi 20 (Unguja ni 15 na Pemba 5).

xviii. Kutayarisha Makala 16 kwa ajili ya Jarida la ARDHI toleo la tano.

xix. Kutoa miongozo ya ujenzi (Planning Policy Guidelines-PPG) 600 ambapo miongozo 480 kwa upande wa Unguja na miongozo 120 kwa Upande wa Pemba.

xx. Kufanya semina na Warsha 8 kwa washirika wa Idara na kutoa elimu kwa wananchi kwenye vipindi 8 vya Redio na TV.

xxi. Kuimarisha kitengo cha utafiti na ushirikiano kwa kuendeleza tafiti 4 Unguja na Pemba 1 juu ya Mipango Miji.

xxii. Kuendelea na hatua za utayarishaji wa Sera, Sheria na Kanuni mpya za Mipango Miji na Maendeleo ya Ardhi.

xxiii. Kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kitovu cha Mji wa Zanzibar (Zanzibar City Cetre- Local Area Plan) katika mradi wa "Green Corridor".

xxiv. Kupanga miji midogo ya Uroa na Pwani Mchangani.

xxv. Kuimarisha maeneo ya miji (Upgrading Schemes) kwa maeneo 7 (Unguja 4 na Pemba 3).

**85. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kuendelea na Programu ya Utambuzi na Usajili wa Ardhi kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania **(MKURABITA)** ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga jumla ya **TZS 420,751,750/=** na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga jumla ya **TZS Bilioni 1.30.** Kazi hii itakapokamilika itasaidia sana kuondosha migogoro ya ardhi Zanzibar.

**BODI YA UHAULISHAJI ARDHI**

**86. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Uhaulishaji inajukumu la kusimamia uhaulishaji (Transfer) wa umiliki wa Ardhi kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwengine. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Bodi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia Uhaulishaji wa ardhi kwa kujadili na kupitisha maombi 1,500 ya uhaulishaji yatakayowasilishwa na kuendesha vikao vya Bodi Unguja na Pemba.

ii. Kutoa Elimu ya Uhaulishaji ardhi kwa wananchi kwa Shehia 12 pamoja na Masheha kuhusu Sheria, Kanuni na Vigezo vya Uhaulishaji.

iii. Kuwajengea uwezo Wajumbe na Watendaji wa Bodi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi ya ndani na nje ya nchi kwa wajumbe na watendaji 7 wa Bodi Unguja na Pemba.

iv. Kuimarisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu za Uhaulishaji utakaosaidia utaratibu bora wa upokeaji na kupitisha maombi ya uhaulishaji wa ardhi.

v. Kuendelea kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Bodi ya Uhaulishaji ili ziendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

**OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

87. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali inajukumu la kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na wananchi kwa ujumla kwa kuhakiki na kuidhinisha kazi zote za uthamini nchini. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuhakiki na kuidhinisha ripoti 300 za uthamini wa rasilimali kwa madhumuni mbalimbali.

ii. Kusajili Wathamini na kuwapatia leseni.

iii. Kutayarisha ripoti za shughuli za uthamini kwa kila robo mwaka zinazofanyika Zanzibar.

iv. Kutayarisha Kanuni ya viwango vya thamani ya ujenzi na Kanuni ya viwango vya thamani ya Ardhi.

v. Kuingiza taarifa za mali zilizofanyiwa uthamini katika mfumo wa kieletroniki.

vi. Kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na kazi zake kupitia vipindi vya Televisheni, Redio pamoja na Mikutano kwa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

88. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 4.218** kwa kazi za kawaida na mishahara.

**PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI**

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuimarisha Makaazi bora na salama, kuanzisha na kuendeleza Miji ya kisasa pamoja na kudhibiti shughuli za ujenzi nchini.

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwepo kwa makaazi bora na kuimarika kwa Miji yetu. Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba, Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi ambapo jumla ya **TZS Bilioni 11.919** zinatarajiwa kutumika ambapo **TZS Bilioni 10.310** ni fedha za Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Viongozi na **TZS Bilioni 1.609** kwa kazi za kawaida. Programu hii imegawika katika programu ndogo kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI**

**90. Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu ndogo hii ni kuwapatia Watumishi wa Umma na Wananchi Makaazi bora pamoja na ujenzi unaozingatia viwango. Matokeo ya muda mfupi (output) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kuwepo kwa makaazi bora ya Viongozi wa umma na wananchi, kuimarika kwa Miji pamoja na Majengo yenye viwango.

**WAKALA WA MAJENGO**

**91. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wakala wa Majengo inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kutoa ushauri elekezi kwa miradi mbalimbali ya Taasisi za Serikali.
ii. Kuzifanyia matengenezo Nyumba 25 za Viongozi wa Serikali ambazo ziko chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo.
iii. Kujenga nyumba mpya 8 za Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ikiwa ni hatua ya awamu ya mwanzo ya ujenzi wa nyumba 20 za Waheshimiwa Mawaziri zinazotarajiwa kujengwa katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo.
iv. Kujenga nyumba mpya 10 za Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar , ikiwa ni hatua ya awamu ya mwanzo ya ujenzi wa nyumba 22 za Makatibu Wakuu zinazotarajiwa kujengwa katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo.
v. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa mujibu wa mpango wa mafunzo.

**SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Shirika la Nyumba Zanzibar katika Programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuanza ujenzi wa jengo jipya la kibiashara na makaazi (G+5) – Kiembe Samaki.
ii. Kuanza ujenzi wa majengo mapya ya Makaazi katika eneo la Kwa Mchina.
iii. Kuzifanyia matengenezo nyumba 32 za Maendeleo zinazomilikiwa na Shirika; Unguja 24 na Pemba 8.
iv. Kuendelea na mradi wa matengenezo makubwa ya nyumba namba 1699-1705 Mnadani.
v. Kuendelea kuzithamini na kuziorodhesha milki za Shirika.
vi. Kukuza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa Shirika.
vii. Kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato ya Shirika.

93. **Mheshimiwa Spika,** ili Shirika la Nyumba Zanzibar liweze kuimarika na kuleta tija zaidi kwa kuwapatia makaazi bora wananchi wa Zanzibar kama ilivyokusudiwa**,** Wizara imeanza mazungumzo na Wawekezaji mbalimbali na Taasisi za Kifedha (Banks) kwa ajili ya kupata mikopo nafuu itakayosaidia kugharamia ujenzi wa nyumba mpya 120 (fleti) za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2025/2026. Aidha Wizara kupitia Shirika la Nyumba inakusudia kupandisha kodi kwa nyumba zake kuanzia mwezi Septemba 2020/2021 kwa kiwango cha asilimia 60 ya bei halisi ya soko kulingana na eneo nyumba ilipo. Hii ni sawa na kutoa punguzo la asilimia 40 ya bei halisi ya soko kwa Wananchi.

94. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika la Nyumba linatarajia kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 3.050** kutokana na kodi za nyumba, mikataba, dhamana, adhabu na nyenginezo. Aidha, Shirika linatarajia kutumia jumla ya **TZS Bilioni 3.658** kwa kazi za kawaida na za Maendeleo.

**BODI YA KONDOMINIO**

**95. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi ya Kondominio imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kufanya usajili wa miradi mipya ya Kondominio.
ii. Kuendelea na usajili wa Nyumba za Maendeleo Unguja na Pemba.
iii. Kufanya ziara za kimafunzo kwa nia ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Bodi pamoja na kukuza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa Bodi;
iv. Kufanya ukaguzi na uhakiki katika miradi inayowasilisha maombi.
v. Kuendelea kufanya ukaguzi kwa miradi ambayo imeshasajiliwa ili kuhakiki uendelezaji wake.
vi. Kusimamia Jumuiya za Kondominio katika uendeshaji na usimamizi wa maeneo ya pamoja kwa nyumba ambazo zishasajiliwa.
vii. Kukusanya na kuhifadhi taarifa za Kondominio.
viii. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuendelea na awamu ya pili ya matengenezo ya jengo la Ofisi na kununua chombo cha usafiri;
ix. Kuendelea kutoa elimu kwa Wadau pamoja na Wananchi kuhusu dhana nzima ya kondominio pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Jumuiya zake;

**BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA**

**96. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutoa elimu kwa taasisi za Serikali na jamii kuhusiana na shughuli, uwezo na majukumu ya kisheria ya Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar.
ii. Kuongeza Ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na Migogoro ya Kodi za Nyumba kwa kuzitolea maamuzi kesi 30 Unguja na Pemba.
iii. Kufanya matengenezo ya Afisi na Ukumbi wa kuendeshea Kesi zinazotokana na migogoro ya kodi za nyumba.

**BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO**

**97. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi Usajili Wasanifu Wahandisi

na Wakadiraji Majengo imepanga kutekeleza Malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na usajili wa Wataalamu wa fani ya ujenzi wa Majengo ,Wahitimu, Mafundi Sadifu na Makapuni ya ushauri wa Ujenzi kama ilivyoainishwa katika Sheria .
ii. Kuendelea kuelimisha Wataalamu wa fani ya Ujenzi kuhusu Ujenzi wa Viwango kwa kufanya Programu 2 za Mafunzo Mafupi .
iii. Kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi na watendaji kwa kuwapatia mafunzo maalaum ya uelewa wa kazi za Bodi.
iv. Kuendelea kufanya ukaguzi wa kazi za Ujenzi wa Majengo zinazofanywa na Wasanifu,Wahandisi na Wakadiriaji Majengo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba kwa lengo la kupata Ujenzi bora na salama.
v. Kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya Nchi zinazofanana na Bodi kwa lengo la kujifunza na kubadilishana ujuzi ili kuleta Maendeleo na ufanisi wa kazi za Bodi.
vi. Kushirikiana na Taasisi za nje zinazotoa misaada kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Misaada la Norway (NORAD) ambazo zitaweza kusaidia kuendeleza mipango mbalimbali ya Bodi hasa program ya kuwaendeleza wahitimu wa fani za Ujenzi.
vii. Kuendelea na mpango wa Mafunzo ya Vitendo (Structure Apprentieceship Program) kwa kwawezesha wahitimu wa fani ya Ujenzi kujiunga na Makampuni mbalimbali nchini kwa lengo la kuwapa ujuzi ili waweze kuwa Wataalamu bora.
viii. Kuhakikisha Jumuiya ya wataalamu iliyosajiliwa inaekewa misingi madhubuti ya ufanyaji kazi na inaendelezwa kwa lengo la kuwaendeleza na kutetea maslahi ya wataalamu walioanishwa katika jumuiya hiyo.

**BODI YA USAJILI WAKANDARASI**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi ya Usajili Wakandarasi imepanga kufanya malengo yafuatayo:-

i. Kusajili Wakandarasi 60 na miradi 120 ya Wakandarasi.
ii. Kuhakikisha shughuli zote za ujenzi nchini zinafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi na zinafuata viwango vya ujenzi (Standard).
iii. Kuandaa semina 4 za mafunzo na mkutano wa Mwaka kwa Wakandarasi.
iv. Kufanya ziara Tanzania Bara kwa nia ya kujifunza na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi.
v. Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya Wakandarasi Unguja na Pemba.
vi. Kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi hasa hesabu na fizikia ili tupate wataalamu wazuri na wa kutosheleza katika fani za ujenzi.
vii. Kufanya mapitio ya Kanuni za Bodi ili kuweza kuwasaidia wakandarasi wadogo na wazalendo katika kufanikiwa kupata kazi za ujenzi.
viii. Kufanya mapitio ya viwango vya ujenzi kwa madaraja mbali mbali ya wakandarasi.
ix. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kununua vifaa vya kazi pamoja na usafiri.

99. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu ya Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naliomba Baraza lakoTukufu kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 10.310** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **TZS Bilioni 1.609** kwa kazi za kawaida.

**HITIMISHO**

100. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia fursa hii ya kuwatumikia Wananchi wenzangu kupitia Wizara hii, ambayo inawagusa wananchi wenyewe ama mmoja mmoja au kwa ujumla wao.

101. **Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kabisa kwamba, utekelezaji wa Wizara yangu ndani ya mwaka unaomalizika ulikabaliwa na changamoto kadhaa kama ilivyoelezwa. Hata hivyo, Wizara ilijitahidi kuzikabili kadri ilivyoweza na kwa kasi. Naamini Wananchi wameona na wameanza kupata matumaini makubwa juu ya utendaji wa Wizara yangu na Serikali ya Awamu ya Nane kwa ujumla. Ninawashukuru sana wananchi kwa uelewa wao,

sambamba na ushirikiano wao wanaonipatia.

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka ujao wa Fedha 2021/2022, wananchi wategemee ongezeko kubwa la ubora wa huduma na ufanisi katika utendaji wa kazi za Wizara yangu ikiwemo usimamizi wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na udhibiti wa ujenzi utakuwa bora zaidi kutokana na mikakati iliyowekwa sambamba na kuimarisha Miji yetu kwa ujenzi wa nyumba za kisasa.

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza, kwa utulivu na kwa umakini wa hali ya juu.

104. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa imani yake kwangu na kunipa nafasi hii muhimu na nyeti ya kuitumikia Nchi yangu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa nasaha, ushauri na maelekezo yao kwangu. Wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awaongezee uadilifu zaidi katika kazi zao, afya na maisha marefu pamoja na familia zao.

Naomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi za Wizara bali pia katika utayarishaji wa Hotuba hii. Shukurani maalumu kwa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa msaada na mashirikiano yao mkubwa kwetu.

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa udhati kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Joseph Kilangi kwa msaada wao mkubwa wanaonipatia. Nawashukuru pia Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizomo chini ya Wizara, Afisa Mdhamini Pemba na Wakurugenzi wote kwa ushirikiano wenu. Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu. Bila ya msaada na ushirikiano wenu kwangu bajeti hii isingeweza kuwasilishwa.

106. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru familia yangu kwa ustahamilivu, Subira na Ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa

majukumu yangu. Kipekee kabisa, namshukuru Mume wangu, wazazi wangu baba na mama, Watoto wangu na familia yangu yote kwa ujumla. Allah awazidishie moyo mwema na mashirikiano makubwa kwangu.

107. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuzishukuru Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali kwa msaada na ushirikiano mkubwa kwa Wizara yangu katika kuhakikisha kwamba majukumu tuliyopewa yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa na kwa ufanisi mkubwa ili kuleta maendeleo kwa wanachi wote wa Zanzibar. Shukurani pia naziwasilisha kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kufikisha habari na taarifa zinazotokana na Wizara yangu.

108. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba sasa waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Tunaimani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2021/2022.

109. **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara yangu iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza hapo juu, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya fedha za Tanzania **Bilioni Nane, Milioni Mia Nane na Saba na Laki Nne (TZS 8,807,400,000)** kwa kazi za kawaida na Mishahara na fedha za Tanzania **Bilioni Kumi, Milioni Mia Tatu na Kumi (TZS 10,310,000,000)** kwa kazi za Maendeleo.

110. **Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Baraza lako Tukufu likubali matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi jumla ya fedha za Tanzania **Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Moja na Kumi na Saba na Laki Nne (TZS 19,117,400,000)** na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya fedha za Tanzania **Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Tisini na Nne, Laki Tatu na Alfu Arubaini na Saba (TZS 1,294,347,000)** kutoka katika vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwa ufafanuzi zaidi naomba muangalie **Kiambatisho “E1 na E2”**

111. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Mheshimiwa Riziki Pembe Juma (MBM)**

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi**

**Zanzibar.**

# VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO "A"**

**MUHUTASARI WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 – MACHI 2021**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2020-MACHI 2021 | ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ofisi kuu Pemba** | 1422008 | Ukodishaji wa Mashine | 2,400,000 | 1,675,000 | 70 |
| | 1422070 | Fii ya Korti | 5,000,000 | 2,462,300 | 49 |
| | **Jumla ndogo** | | **7,400,000** | **4,137,300** | **56** |
| **Wakala wa Majengo** | 1415011 | Ukodishwaji wa Mashine | 500,000 | 174,000 | 35 |
| | 1422077 | Mapato ya Kazi za Biashara | 5,000,000 | 7,720,000 | 154 |
| | **Jumla ndogo** | | **5,500,000** | **7,894,000** | **144** |
| **Kamisheni ya Ardhi** | 1422093 | Valuation Fee | 40,000,000 | 51,363,700 | 128 |
| | 1422028 | Muongozo wa Matumizi ya Ardhi | 25,000,000 | 25,096,424 | 100 |
| | 1422008 | Nyaraka za Ardhi | 215,000,000 | 181,594,192 | 84 |
| | 1422043 | Ada ya Upimaji na Ramani | 220,000,000 | 193,712,640 | 88 |
| | 1422074 | Kodi ya usajili wa Ardhi | 35,000,000 | 64,764,550 | 185 |
| | | **Jumla ndogo** | **535,000,000** | **516,531,506** | **97** |
| **Mahkama ya Ardhi** | 1422072 | Fii ya Korti | 7,100,000 | 7,400,000 | 104 |
| | **Jumla ndogo** | | **7,100,000** | **7,400,000** | **104** |
| | **JUMLA KUU** | | **555,000,000** | **535,962,806** | **97** |

**KIAMBATISHO "B"**

## MUHUTASARI WA MATUMIZI YA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 – MACHI 2021

| Na. | PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | IDARA/ TAASISI | MAKISIO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi | **1.** Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 328,670,000 | 268,027,000 | 139,880,415 | 52.19 | 42.56 |
| | | **2.** Utawala na Uendeshaji | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2,155,578,260 | 1,794,204,000 | 1,171,579,567 | 65.30 | 54 |
| | | **3.** Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Ofisi Kuu Pemba | 612,302,160 | 493,462,000 | 487,285,520 | 98.75 | 79.58 |
| | | **Jumla ndogo** | | **3,096,550,420** | **2,555,693,000** | **1,798,745,502** | **70** | **58** |
| | | **1.** Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | Mahakama ya Ardhi | 668,874,400 | 572,677,000 | 241,157,385 | 42.11 | 36.05 |
| 2 | Utawala wa Ardhi,Nyumba na Makaazi | **2.** Utawala wa Ardhi na Makaazi | Kamisheni ya Ardhi | 2,776,000,000 | 2,082,672,000 | 1,392,946,949 | 66.88 | 50.18 |
| | | | Afisi ya Mtamini Mkuu wa Serikali | 132,000,000 | 99,000,000 | 40,882,000 | 41.29 | 30.97 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Bodi ya Uhaulishaji Ardhi | 1,717,000,000 | 1,287,854,000 | 211,000,000 | 16.38 | 12.29 |
| | | | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 186,000,000 | 142,425,000 | 42,035,850 | 29.51 | 22.60 |
| | | | Bodi ya Kondominio | 200,000,000 | 150,000,000 | 51,300,000 | 34.20 | 25.65 |
| | | | Wakala wa Majengo | 380,010,000 | 289,000,000 | 93,956,650 | 32.51 | 24.72 |
| | | | Bodi ya Usaji Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo | 793,280,000 | 594,961,000 | 128,730,474 | 21.64 | 16.23 |
| | | | Bodi ya Usajili Wakandarasi | 359,601,000 | 269,700,750 | 203,655,474 | 75.51 | 56.63 |
| | | **Jumla ndogo** | | **7,212,765,400** | **5,488,289,750** | **2,405,664,782** | 43.83 | 33.35 |
| | | **JUMLA KUU** | | **10,309,315,820** | **8,043,982,750** | **4,204,410,284** | 52.27 | 40.78 |

**KIAMBATISHO “C1”**

## MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2020/2021

| NAM | TAASISI | W'UME | | W'KE | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | |
| 1 | UTUMISHI NA UENDESHAJI | - | - | - | - | 0 |
| 2 | MIPANGO SERA NA UTAFITI | 2 | - | - | - | 2 |
| 3 | KAMISHENI YA ARDHI | 31 | - | 15 | - | 46 |
| 4 | MAHAKAMA YA ARDHI | 9 | - | 3 | - | 12 |
| 5 | MTHAMINI MKUU WA SERIKALI | 1 | - | - | - | 1 |
| 6 | SHIRIKA LA NYUMBA | 14 | - | 15 | - | 29 |
| 7 | WAKALA WA MAJENGO | 3 | - | 2 | - | 5 |
| **JUMLA KUU** | | **61** | | **35** | | **96** |

**KIAMBATISHO "C2"**

**MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA WAFANYAKAZI WA**

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2020/2021**

| Na. | TAASISI | AINA YA MAFUNZO | W'UME | W'KE | JUMLA | CHUO | TAREHE YA KUMALIZA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **UTUMISHI NA UENDESHAJI** | Degree in Record and Achieve Management | 1 | 0 | 1 | Institute of Public Administration (IPA) | 2022 |
| | | Degree in Human Resources Management | 1 | 0 | 1 | Mwalim Nyerere Memorial | 2022 |
| | | Diploma in Record and Achieve Management | 0 | 1 | 1 | ICPS | 2021 |
| 2 | **MIPANGO SERA NA UTAFITI** | Master of Project Planning Monitoring and Evaluation | 0 | 1 | 1 | Institute of Rural Development Planning | 2021 |
| 3 | **KAMISHENI YA ARDHI** | Master of Urban Planning | 1 | 0 | 1 | China | 2021 |
| | | Diploma in Mechanical Engineering | 1 | 0 | 1 | Karume Institute of Science and Technology (KIST) | 2021 |
| | | Degree of Environmental Planning and Management | 1 | 0 | 1 | Institute of Rural Development Planning | 2023 |
| | | Degree of gender development | 0 | 1 | 1 | Mwalim Nyerere Memorial | 2021 |
| | | Master of Urban Planning | 0 | 2 | 2 | Ardhi University | 2021 |
| | **KAMISHENI YA ARDHI (PEMBA)** | Degree in Land Scape Architecture | 0 | 1 | 1 | Ardhi University | 2023 |
| | | Recording Management | 1 | 0 | 1 | IPA | 2021 |
| | | Degree in Public Administration | 1 | 0 | 1 | Open University | 2023 |
| | | Master of Monitoring and Evaluation | 1 | 0 | 1 | Open University | 2021 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | **MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | Master of Science in real Estate Business | 0 | 1 | 1 | Ardhi University | 2022 |
| | | Bachelor Degree in Human Resource Management | 0 | 1 | 1 | Kampala University | 2023 |
| 5 | **SHIRIKA LA NYUMBA** | PhD of Economics | 1 | 0 | 1 | Poltava University of Ukraine | 2022 |
| | | Degree of Architecture | 0 | 1 | 1 | Ardhi university | 2025 |
| | | Diploma ya Fundi Umeme | 1 | 0 | 1 | KIST | 2022 |
| | **SHIRIKA LA NYUMBA (PEMBA)** | Certificate in Electrical Stage Three | 1 | 0 | 1 | KIST | 2022 |
| | | Degree in Human Resources Management | 1 | 0 | 1 | Open University | 2023 |
| | | Degree in Public Administration | 1 | 0 | 1 | Open University | 2023 |
| 6 | **WAKALA WA MAJENGO** | Certificate in International Relations | 1 | 0 | 1 | IPA | 2022 |
| | | Certificate in Electrical | 0 | 1 | 1 | KIST | 2022 |
| | | Certificate in Driving Stage Three/VIP | 1 | 0 | 1 | NIT | 2022 |
| | **WAKALA WA MAJENGO (PEMBA)** | Diploma in Public Administration | 1 | 0 | 1 | Center for Professional and Vocational Training | 2023 |
| | | Certificate in Electrical | 1 | 0 | 1 | JKT Mgulani Dar-es Salaam | 2023 |
| | | Degree in Quantity Surveyor and Construction Economic | 1 | 0 | 1 | Ardhi University | 2024 |
| **JUMLA KUU** | | | **16** | **9** | **25** | | |

**KIAMBATISHO “D”**

## MIRADI YA UJENZI ILIYOSIMIAMIWA NA WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

## KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 – MACHI 2021

| Na. | AINA YA KAZI NA AFISA / MAOFISA WANAOSIMAMIA. | TAASISI | MAJUKUMU YA ZBA | MAHALA PA KAZI | MAELEZO YA UTEKELEZAJI . |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Ukuta wa kuzuia Maji ya Bahari | Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | Kusimamia na Kujenga kwa kushirikiana na Mtaalamu kutoka Shirika la Bandari | Msuka - Pemba. | Mkataba umeshasainiwa. Kinachosubiriwa ni Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. |
| 2. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Jengo la Utawala IPA. | IPA | Pre – Contract (Kutayarisha Ramani za Ujenzi na BoQ) | Tunguu | Utayarishaji wa Ramani na na BoQ unaendelea. |
| 3. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Kituo cha Afya IPA. | IPA | Pre – Contract (Kutayarisha Ramani za Ujenzi na BoQ) | Tunguu | Utayarishaji wa Ramani na na BoQ unaendelea. |
| 4. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Nyaraka. | PBZ. | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Mwanakwerek we. | Utayarishaji wa Ramani na BoQ unaendelea |
| 5. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ukarabati wa Tawi la Benki Forodhani. | PBZ | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Forodhani | Utayarishaji wa Ramani na na BoQ unaendelea |
| 6. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). | Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Maisara – Unguja. | Utayarishaji wa Ramani za Ujenzi pamoja na Nyaraka za Zabuni unaendelea. Makubaliano ya Mkataba |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | bado hayajafanyika. |
| 7. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Chuo cha Sheria cha Mahakama Kuu Zanzibar. | Ofisi ya Rais - KSUUB | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Tunguu. | Utayarishaji wa Ramani za Ujenzi pamoja na Nyaraka za Zabuni unaendelea. |
| 8. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Bohari ya Madawa ya Wizara ya Afya. | Wizara ya Afya Zanzibar. | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Marhubi | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea. |
| 9. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani Chamanagwe. | Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda. | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chamanagwe | Utayarishaji wa Ramani za Ujenzi pamoja na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 10. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA ). | ZAECA | Pre-Contract na Post Contarct (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni pamoja na kusimamia Ujenzi) | Migombani | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea. |
| 11. | Matayarisho ya Nyaraka kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Shirika la Bandari Mkoani – Pemba. | Shirika la Bandari Zanzibar | Pre-Contract na Post Contarct (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni pamoja na kusimamia Ujenzi) | Mkoani – Pemba. | Tunasubiri kupata Site plan mpya ili tuendelee na taratibu za kutayarisha Ramani na Nyaraka za Zabuni. |
| 12. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira - ZEMA. | Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Maruhubi | Kazi imeshaanza lakini bado tunasubiria hatua za kusaini Mkataba. |
| 13. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi Rais- Kazi, Uchumi na Uwekezaji. | Afisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni pamoja na kusimamia Ujenzi) | Mwanakwerekwe | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea. |
| 14. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ukarabati wa Jengo la Kupokelea Abiria | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | AAKIA | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unasubiri kupatiwa hadidu rejea kutoka |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | AAKIA (Terminal II) | | | | kwa Client. |
| 15. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Jengo la Makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais Dodoma. | VP II | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Dodoma. | Kazi inaendelea. |
| 16. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi na Maabara ya Dawa na Chakula | ZFDA. | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chamanangwe | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 17. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Jengo la Afisi ya Bodi ya Uhaulishaji. | Bodi ya Uhaulishaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Gombani Pemba | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 18 | Matayarisho ya Nyaraka za Extension ya Jengo la Uhamiaji Chake Chake Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chake Chake | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 19. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi wa Jengo la Idara ya Uhamiaji Mkoani Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Mkoani | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 20. | Matayarisho ya Nyaraka za Ukarabati wa Jengo la Kupumzikia (Rest House) Idara ya Uhamiaji Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chake Chake na Mkoani | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 21. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi wa Uzio wa Nyumba ya Idara ya Uhamiaji (VIP Main House) Pagali Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chake Chake | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 22. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi wa Afisi ya Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Wete na Micheweni | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 23. | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi wa Mkahawa wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini Pemba. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Wete | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 24. | Matayarisho ya Nyaraka za Ukarabati wa Nyumba za Wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji Micheweni. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Micheweni | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 25. | Matayarisho ya Nyaraka za Ukarabati wa Uzio wa Ofisi ya Idara ya Uhamiaji Micheweni. | Uhamiaji | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Micheweni | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 26. | Matayarisho ya Nyaraka za Ukarabati wa Jengo la Mpiga Chapa wa Serikali. | ZAGPA | Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni) | Chake Chake | Utayarishaji wa Ramani na Nyaraka za Zabuni unaendelea |
| 27. | Usimamizi wa Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. | Wizara ya Afya. | Post Contract (Kusimamia Kazi ya Ujenzi) | Maruhubi. | Ujenzi unaendelea katika hatua ya utekelezaji na kazi hiyo inatekelezwa na Kampuni ya M/s Shamjo. |
| 28. | Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya Mkokotoni na Kama Unguja. | Wizara ya Vijana | Post Contract (Kusimamia Kazi ya Ujenzi) | Mkokotoni | Ujenzi unaendelea na kazi hiyo inatekelezwa na Wakala wa Barabara |
| 29. | Ujenzi wa Chuo cha Amali Makunduchi Unguja | Wizara ya Elimu Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Makunduchi | Ujenzi unaendelea na unatekelezwa na Kampuni ya M/s Mindset Tech. |
| 30. | Ujenzi wa Maabara ya Kisasa ya ZFDA Mombasa | ZFDA | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Mombasa | Ujenzi Unaendelea na unatekelezwa na Kampuni ya M/s QBC ya Zanzibar |
| 31. | Ukarabati wa Jengo la kuzuia Madawa ya Kulevya. | Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Migombani | Ukarabati haujaanza |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 32. | Ujenzi wa Jengo la TRA Mayugwani | TRA | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Mayugwani | Ujenzi unaendelea na unatekelezwa na Kampuni ya Associated Investment Services LTD na sasa tumo kwenye muda wa uangalizi (Defect liability Period) |
| 33. | Ujenzi wa Kijiji cha Wananchi Dundua | ZURA | Post Contarct (Kusimamia Ujenzi) | Dundua | Kazi ya Ujenzi imemalizika na sasa tuko kwenye kipindi cha uangalizi (Defect liability Period) ya mwaka mmoja. |
| 34. | Ujenzi wa Ukuta kuzunguka eneo la Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu (IPA) | Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu (IPA) | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Tunguu | Ujenzi umekamilika na kazi hiyo imetekelezwa na Chuo cha Mafunzo na sasa tupo kwenye kipindi cha uangalizi (Defect liability Period) ya mwaka mmoja |
| 35. | Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake | Wizara ya Afya Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Chake Chake Pemba. | Ujenzi unaendelea na unatekelezwa na Kampuni ya M/s RANS |
| 36. | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Jeshi la Uhamiaji Kivunge | Idara ya Uhamiaji Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Kivunge | Ujenzi unaendelea na kazi hii inatekelezwa na Kampuni ya M/s Albatna |
| 37. | Ukarabati wa Soko la Samaki Nungwi (MRADI WA SWOFISH) | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Nungwi | Kazi imekamilika na imo kwenye kipindi cha uangalizi na inatekelezwa na Kampuni ya M/s Grasshopper ya Zanzibar |
| 38. | Ukarabati wa Soko la Samaki Tumbe (MRADI WA SWOFISH) | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Tumbe | Kazi imekamilika na imo kwenye kipindi cha uangalizi na inatekelezwa na Kampuni ya M/s. KIN Investment ya Pemba. |
| 39. | Ujenzi na Ukarabati wa | Wizara ya | Post Contract (Usimamizi wa | Kizimbani | Ujenzi umesimama |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Maghala ya ZALIRI Kizimbani | Kilimo Zanzibar | Ujenzi) | | |
| 40. | Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Malindi | Ujenzi umesimama |
| 41. | Ukarabati wa Maghala ya Donge, Kibokwa na Kilombero | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Donge, Kibokwa na Kilombero | Ujenzi umesimama |
| 42. | Ujenzi wa Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais Pagali Pemba | Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar. | Pre-Contract na Post Contarct (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni pamoja na kusimamia Ujenzi) | Pagali Pemba | Ujenzi Umekamilika |
| 43. | Ujenzi wa Bohari ya Dawa Vitongoji | Wizara ya Afya Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Vitongoji | Ujenzi unaendelea |
| 44 | Ujenzi wa Ukuta na “Landscaping” Bohari ya Dawa Vitongoji | Wizara ya Afya Zanzibar | Post Contract (Usimamizi wa Ujenzi) | Vitongoji | Ujenzi unaendelea |
| 45. | Ujenzi wa Vibanda vya Kukagulia Wageni wanaoingia katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA | Uhamiaji | Post Contarct (Kusimamia Ujenzi) | AAKIA | Kazi inaendelea na inatekelezwa na M/s SHAMJO |
| 46. | Ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Viwango Zanzibar | ZBS | Karani wa Ujenzi (Clerk of Works) | Marhubi | Ujenzi unaendelea |
| 47. | Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Kwahani | Wizara ya Fedha Zanzibar | Karani wa Ujenzi (Clerk of Works) | Kwahani | Ujenzi unaendelea |
| 48. | Ujenzi wa Mahakama Kuu | Mahakama Kuu Zanzibar | Karani wa Ujenzi (Clerk of Works) | Tunguu | Ujenzi unaendela |
| 49. | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya ZRB Pemba | Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) | Karani wa Ujenzi (Clerk of Works) | Gombani-Pemba | Ujenzi unaendelea |

**KIAMBATISHO “E1”**

## MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

| Na. | PROGRAMU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI/IDARA | MAKISIO KWA MWAKA | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KAZI ZA KAWAIDA** | **RUZUKU** | **KAZI ZA MEANDELEO** | **JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA** |
| 1 | 1. Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | **1.** Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 305,400,000 | - | - | 305,400,000 |
| | | **2.** Utawala na Uendeshaji | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,928,280,000 | - | - | 1,928,280,000 |
| | | **3.** Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Afisi Kuu Pemba | 746,600,000 | - | - | 746,600,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | **2,980,280,000** | - | - | **2,980,280,000** |
| 2 | Usimamizi wa Ardhi | **1.** Usimamizi wa Ardhi | Kamisheni ya Ardhi | - | 2,632,500,000 | - | |
| | | | Bodi ya Uhaulishaji Ardhi | - | 850,000,000 | - | 850,000,000 |
| | | | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | - | 151,800,000 | - | 151,800,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mahakama ya Ardhi | 583,820,000 | - | - | 583,820,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | **583,820,000** | **3,634,300,000** | - | **4,218,120,000** |
| 3 | Maendeleo ya Makaazi | **1.** Maendeleo ya Makaazi | Wakala wa Majengo | **-** | 350,000,000 | 10,310,000,000 | 10,660,000,000 |
| | | | Bodi ya Kondominio | - | 234,000,000 | - | 234,000,000 |
| | | | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | - | 130,000,000 | - | 130,000,000 |
| | | | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo | - | 631,800,000 | - | 631,800,000 |
| | | | Bodi ya Usajili Wakandarasi | - | 263,200,000 | - | 263,200,000 |
| | | | **Jumla ndogo** | **-** | **1,609,000,000** | **10,310,000,000** | **11,919,000,000** |
| | | | **JUMLA KUU** | **3,564,100,000** | **5,243,300,000** | **10,310,000,000** | **19,117,400,000** |

**KIAMBATISHO “E2”**

**MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | 1422008 | Ukodishaji wa Mashine | 15,000,000 |
| | 1422070 | Fii ya Korti | 5,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **20,000,000** |
| **WAKALA WA MAJENGO** | 1415011 | Ukodishaji wa Mashine | 15,000,000 |
| | 1422077 | Mapato ya Kazi za Biashara | 35,000,000 |
| | 1430009 | Ada ya ushauri elekezi | 200,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **250,000,000** |
| **KAMISHENI YA ARDHI** | 1422093 | Valuation fee | 60,000,000 |
| | 1422028 | Muongozo wa Matumizi ya Ardhi | 40,000,000 |
| | 1422008 | Nyaraka za Ardhi | 320,000,000 |
| | 1422043 | Ada ya upimaji na Ramani | 350,000,000 |
| | 1422074 | Kodi za Usajili wa Ardhi | 60,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **830,000,000** |
| **MAHAKAMA YA ARDHI** | 1422072 | Fii ya Korti | 7,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **7,000,000** |
| **OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | 1422093 | Ada ya Uthamini | 50,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **50,000,000** |
| **BODI YA KONDOMINIO** | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 137,347,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **137,347,000** |

| | | |
|---|---|---|
| | **JUMLA KUU** | **1,294,347,000** |